# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA
# SHULE YA SEKONDARI OMUMWANI
# S.L.P 217.  BUKOBA

SIMU:

**1. 0626828832-- MKUU WA SHULE**
**2.0782649433 – MAKAMU MKUU WA SHULE**
**3.0620208824 –MWL. TAALUMA**
**4. 0788353338- MWL. NIDHAMU**
**5. 0756072226 - MATRON**
**6. 0758127474 – PATRON**
**7. 0765980730 – MHASIBU**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………..
…………………………………
S.L.P…………………………
……………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANOSHULE YA SEKONDARI OMUMWANI MWAKA ……….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shulehii kwa mwaka ……. kwa Tahasusi ya ……………………….

Shule ya Sekondari Omumwani ipo umbali wakilometa 2 ½ Kaskazini mwa mji wa Bukoba. Usafiri wapikipiki na tax kutoka mjini kufika shuleni unapatikana stendi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **……….**
Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………… **na** mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………..**

## 1. MICHANGO MBALIMBALI

Mchanganuo ufuatao ni wa malipo ya michango mbalimbali.

| S/N | MALIPO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho na picha | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya shule | 5,000/= |
| | JUMLA | 80,000/= |

Fedha zote zilipwe katika akaunti ya shule namba **31810017213** yenye jina la **OMUMWANI SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT** ya **NMB**. Ni lazima mwanafunzi afike shuleni na stakabadhi ya malipo (Bank pay – in – slip) ambayo Itawasilishwa kwa mhasibu wa shule na mzazi atapatiwa stakabadhi. Andika majina sahihi yamwanafunzi na mchepuo atakaosoma katika stakabadhi ya malipo.

## 2. SARE YA SHULE

A: Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare zifuatazo**:-**

| S/N | AINA YA NGUO | |
|---|---|---|
| 1. | Sketi mbili za rangi ya "dark blue" urefu wake kama unavyoonekana kwenye picha iliyoambatanishwa (linda box) | Picha imeambatanishwa |
| 2. | Sketi moja nyeusi kwa ajili ya kushindia baada ya masomo urefu kama inavyoonekana kwenye picha. | |
| 3. | Sweta moja ya rangi ya kijivu iliyoiva, yenye michilirizi nyeupe mikoani na shingoni V ikiwa na nembo ya shule upande wa kushoto | Picha imeambatanishwa |
| 4. | Tai moja ya rangi ya dark blue (ndefu) yenye michirizi myeupe | Picha imeambatanishwa |
| 5. | T-shirt mbili zenye nembo ya shule **Zinapatikana shuleni.** | |
| **6** | Gauni moja rangi ya pinki kwa ajili ya siku ya shamba,**mshono wa solo** | Picha imeambatanishwa |
| **7** | Shati 2 nyeupe zenye mikono mirefu. Ukiweza kupata halua ni vema zaidi. | |

**N:B : Kwa mzazi yeyote atakayepata mkanganyiko juu ya sare zilizotajwa apige simu kati ya namba zilizoorodheshwa ili kupata maelekezo zaidi kabla ya manunuzi ili kuondoa kununua sare isiyo sahihi.**

## A. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Mwanafunzi anatakiwa afike shuleni akiwa na sare na mahitaji mengine kama ilivyoainishwa hapa chini;

| S/N | MAHITAJI MENGINE |
|---|---|
| 1. | Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye jumla ya matundu yasiyozidi 10 na yasiyopungua 8 vyenye visigino vifupi. |
| 2. | Soksi ndefu nyeupe jozi tatu |
| 3. | Bukta moja rangi pink na T- shirt yake pamoja na skin tait nyeusi kwa ajili ya michezo isiyokuwa na maandishi yoyote |
| 4. | "Truck suit" nzito ya Dark Blue (kampuni ya Adidas) kwa ajili ya usiku, isiwe na kofia |
| 5. | Raba nyeupe kwa ajili ya michezo |
| 6. | Godoro moja futi 2 ½ kwa 6 |
| 7. | Mashuka mawili ya rangi ya blue na blanketi moja (yawekewe alama) |
| 8. | Mto na foronya moja ya rangi ya blue |
| 9. | Chandarua kimoja hiki ni kwa lazima (kiwe cha duara) |
| 10. | Ndoo 2 lita 10 zenye mfuniko. |
| 11. | Taulo, malapa, sabuni za kutosha, vitenge viwili, mswaki na dawa ya meno (Vikoi na yeboyebo/crocks haviruhusiwi) |
| 12. | Sahani, Bakuli, kikombe na kijiko |
| 13. | "Toilet papers" za kutosha |
| 14. | Mwamvuli |
| 15. | Sanduku moja imara la chuma (trank) |
| 16. | Sanitary pads (pedi) za kutosha |
| 17. | Vibanio vya kutosha kwa ajili ya kuanikia nguo (angalau 20) |

- Hakikisha vifaa vyote/nguo vimewekewa alama kuondoa upotevu.

***N.B.***

1. **Nguo nyingine zozote haziruhusiwi kabisa shuleni**

2. Wanafunzi wanaovaa ushungi, wa darasani uwe na rangi nyeupe, wa kuvaa baada ya masomo uwe wa rangi ya nyeupe urefu wake usifunike kiwiko cha mkono. **Ushungi wenye urefu unaozidi kiwiko chamkono na mitandio haitaruhusiwa**. Hivyo mzazi hakikisha mwanao anashona kulingana na vipimo.

## 3. MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA.

1. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
3. Mkebe wa Hisabati (Mathematical set) na scientific calculator (kwa michepuo ya sayansi na jiografia)
4. “Dissecting kit” kwa wanafunzi wa masomo ya elimu ya viumbe (BIOLOGY).
5. Stop watch kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi
6. Counter books kumi (Quire three) kwa ajili ya masomo darasani.
7. **Kadi ya bima ya afya ni lazima** kuja nayo siku ya kuripoti na iwe ni bima inayofanya kazi sehemu yoyote au mwanafunzi aje na shilingi elfu hamsini na mia nne (50,400.00) kwa ajili ya kukatiwa bima.
8. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika. (Orodha na majina ya vitabu mbalimbali yameambatishwa)
9. Kalamu za wino, rula 2 (ngumu yenye sentimita 30) na penseli za kutosha
10. Ream mbili 2 za karatasi aina ya A4 iliyoandikwa **double A** isiyo ya mistari.
11. Sabuni ya maji lita 5 aina ya Dexi
12. Graph padi 1 yenye kurasa 50 (kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na jiografia
13. Box file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mitihani(mali ya mwanafunzi)
14. Kila mwanafunzi aje na taa ya sola kwa matumizi yake binafsi umeme unapokatika (iwekewe alama). Hii ni lazima
15. Picha 2 za passport size. Akiwa amevaa shati la shule na nywele zikiwa fupi. Kama anavaa ushungi, uwemweupe na sura ionekane (ziandikwe majina na tahasusi nyuma)
16. Begi la kubebea vitabu./ madaftari lisiwe lenye picha au michoro.

## 4. VIFAA VYA USAFI

Ili kuwafundisha na kuwajenga wanafunzi wetu katika tabia ya usafi na utunzaji wa mazingira na pia kuwekashule yetu katika hali ya usafi na mazingira ya kuvutia, mwanafunzi afike shuleni akiwa na vifaa vifuatavyo:

| S.Na | TAHASUSI | KIFAA CHA USAFI |
|---|---|---|
| 1 | PCM | Kotama na fyekeo na hard broom<br>Jembe lenye mpini |
| 2 | PCB | Squizer, panga jembe lenye mpini. |
| 3 | CBG | Fagio za chelewa zisizo za kusimama na kotama na hard broom (ufagio mgumu wa plastic), jembe lenye mpini. |
| 4 | HGE | Jembe na mpini wake na kotama, squizer, hardbloom. |
| 5 | HGL | Squizer, chelewa na kotama, brush za sink na |

| | | |
|---|---|---|
| | | jembe lenye mpini. |
| 6 | HGK | Fyekeo, hard broom, kotama na jembe lenye mpini. |
| 7 | HKL | Hard broom, kotama, fyekeo na jembe lenye mpini wake. |
| 8 | HGLi | Hard broom, kotama, chelewa na jembe lenye mpini wake. |
| 9 | HGFi | Hard broom, kotama, chelewa na jembe lenye mpini wake. |

## 5. VIAMBATISHO

Hakikisha unasoma na kujaza viambatisho vifuatavyo:-

- Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi (**Ijazwe katika hospitali ya wilaya/Mkoa)**
- Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Hakikisha imejazwa na kukamilika).
- Sheria za shule.

## 6. SIKU YA KURIPOTI SHULENI

- Kila mwanafunzi aje amevaa Sketi nyeusi iliyoshonwa sawa na ya dark blue na shati jeupe la mikono mirefu, pamoja na viatu na soksi
- Siku za kuripoti ni Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 mchana (muda wakazi).
- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka, kila mwanafunzi aje amenyoa na sio kunyoa kiduku.

## 7. UTARATIBU WAKATI WA LIKIZO

- Mwanafunzi atatakiwa kwenda likizo zote fupi za wiki 2 na ndefu za wiki 4 kama kutakuwepo na utaratibu mwingine mzazi atashirikishwa.

- Mzazi atawajibika kumugharamia nauli ya kwenda na kurudi bila kisingizio chochote.

Mwisho, napenda kumkaribisha mwanao katika Shule ya Sekondari ya Omumwani, mahali ambapo tumelenga kutoa elimu na malezi bora kwa wasichana ambao ni wajenzi wa Taifa letu la Tanzania kwa siku zijazo. Mwanafunzi ajiandae kwa moyo na ari ya kutaka kuelekezwa, kufundishwa na kujifunza. Nidhamu, utii, heshima, uwajibikaji na kujituma ni mambo muhimu na ya msingi sana yanayotiliwa mkazo na kusisitizwa katika shule yetu wakati wote.

## 8. USALAMA WA WANAFUNZI WAKATI WA SAFARI

Mzazi unawajibika kuhakikisha mwanao anakuwa salama awapo safarini aidha ili kuhakikisha mwanafunzi anafika salama shuleni tumeambatanisha namba za simu za waendesha pikipiki na dereva tax tunaowafahamu ili kuondoa usumbufu hasa kwa wanafunzi watakaofika usiku.

**Dereva wa pikipiki (bodaboda)**

1. Erick John- 0711967714
2. Moses Mbaluki- 0684356436
3. Adelius Mzee- 0620873222

**Dereva Tax**

1. Remigius Kaiza 0754529980/0684529980

Nakutakia mafanikio mema na karibu sana katika shule ya Sekondari ya Omumwani.

**……………………**
**JULIANA J. LUKWETO**
**MKUU WA SHULE.**

**KIAMBATISHO A.**

## 1. MEDICAL EXAMINATION FORM

DATE…………………………NAME OF STUDENT…………………………………………………

To medical officerof……………………… District/Regional;/Referral/Designated

Hospital:

P.O.BOX …………………………………

Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for Beingable to pursue two years of Secondary school Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with specialneeds:-

i. Blood pressure …………………………………………………………

ii. Sickle cell test ………………………………………………………….

iii. (a) Eyesight ……………………………………………………..… ……..

(b) Hearing ………………………………………………………........................

(c) Spleen ……………………………………………………………………………

(d) Limps ………………………………………………………………………….

(e) Venereal diseases ……………………………………………………………..

(f) Leprosy……………………………………………………………………….

(g) Epilepsy………………………………………………………..………………..

(h) Typhoid ……………………………………………………………………...

iv. N e u r o s e s … ………………………………………………………………...

v. O t h e r s e r i o u s d i s e a s e s ………………………………………..……………..

vi. Pregnancy: ……………………………………………………………………………

General comment (s)…………………………………………………………………………

Name…………………………………………Signature……………………………...

Designation ……………………………………………………………………………..

Official stamp…………………………………………………………………………

Date ………………………………………………………………………………………..

***ANGALIZO: Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina nasahihi ya mganga .Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuwa vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.***

**KIAMBATISHO B**

**2. MAELEZO BINAFSI YA**

**MWANAFUNZIHABARI ZA**

**MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanfunzi ……………………………………………………………….…
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………...
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa …………………………….. Wilaya ……………………...
   Tarafa …………………….. Kata ……………….. Kijiji/Mtaa…………………………
4. Dini …………………………… Dhehebu ……………………………………………..

**HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la baba mzazi/mlezi ………………………………………………………
   Anuani ………………………………… Namba ya simu ……………………….
   Kazi ya baba mzazi/mlezi ……………………………………………………...
   Yuko hai? Ndio/Hapana (Kata isiyohusika)

2. Jina la Mama mzazi/mlezi ……………………………………………………..
   Anuani ……………………………….. Namba ya simu ………………………...
   Kazi ya mama mzazi/mlezi ……………………………………………………
   Yuko hai? Ndiyo/Hapana (kata isiyohusika)

Picha ya baba mzazi/mlezi

Picha ya mama mzazi/mlezi

3. Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa zamatatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.

1. Jina kamili ……………………………………… Anuani ……………………
   Namba ya simu ………………………………………………………………
   Kazi yake …………………………… Uhusiano na mwanafunzi………………...

Picha ya ndugu wa karibu

2. Jina kamili la mtendaji…………………………………………………………………….

   Namba ya simu ……………………………………sahihi na muhuri…………………...

**NB: Hakikisha sehemu hii inasainiwa na kuwekewa muhuri na mtendaji wa kijiji/mtaa unakoishi.**

## KIAMBATISHO C

## 3. SHERIA ZA SHULE.

Sheria na kanuni mbalimbali hutumika kama miongozo ya kumwezesha anayeishi katika jumuiya yoyote kuwa na mahusiano mazuri na wenzake kwa kumwekea mipaka ya kiutendaji pamoja na kusimamia uhuru ambao ukizidi kiwango unaweza kuleta madhara. Aidha, miongozo hii humwezesha mlengwa kukua na kuendelea kwa kuimarisha uhusiano mzuri wa kila siku katika jamii inayomzunguka ambapo kila mmoja hukubali kuzifuata bilakuacha. Sheria na kanuni huainisha bayana haki na wajibu wa kila mmoja katika jamii au taasisi husika. Hata hivyo, adhabu kwa atakayekiuka au kwenda kinyume na sheria au kanuni zilizokubaliwa na jumuiya au taasisi husika huwekwa ili kuleta nidhamu na maendeleo ya pamoja. Hivyo, kama kila mmoja katika jumuiya husika atazishika na kufuata sheria na kanuni zilizokubalika katika eneo lake kwa moyo mkunjufu, maisha huwa bora, yenye amani tele na furaha.

Kwa mtazamo huu, shule ya Sekondari ya Omumwani inazo sheria rahisi sana zinazoelekeza haki na wajibu wa mwanafunzi atakayechaguliwa kujiunga na shule hii ili aweze kutimiza malengo yake ya kusoma na kufaulu na hatimaye akajenge familia na Taifa lake. Adhabu ya ukiukwaji wa sheria hizi pia zimewekwa bayana ambapo mzazi na mwanafunzi wanatakiwa kuzisoma na kuzielewa.

- **HAKI ZA MWANAFUNZI**

Mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Omumwani anazo haki zifuatazo:

1. Kufundishwa masomo aliyochagua kwa idadi ya vipindi na muda ulioanishwa katika muhtasari wa kilasomo.
2. Kupewa majaribio, mazoezi na mitihani ya kujipima uelewa wake katika masomoaliyofundishwa
3. Kuomba ufafanuzi kwa Mwalimu husika kwa kutumia taratibu zilizowekwa na shule kama hakupewa majaribio na mazoezi ya kutosha kulingana na utaratibu, kanuni na sheria za shulena taratibu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
4. Kupatiwa mahali safi na salama pa kulala kwa muda wote awapo shuleni.
5. Kupata mlo wakutosha kwa nyakati zote zinazotakiwa kama ilivyoanishwa katika ratiba ya shule.
6. Kupata matibabu wakati anapougua kwa kufuata taratibu zilizopo shuleni.
7. Kulindwa dhidi ya ajali wakati wote awapo shuleni.
8. Kuadhibiwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake au kufuata sheria na taratibu za shule hii au za nchi.

- **WAJIBU WA MWANAFUNZI**

(i) Kujifunza kwa bidii na maarifa ili kufaulu masomo yote anayosoma kwa kiwango Cha alama 65% na kuendelea kwa kila mtihani.(kifungu hiki kimewekewa mkataba utakaosainiwa shuleni siku ya kuripoti.

(ii) Kutii kwa moyo wa dhati sheria za nchi, za serikali za mitaa, kijiji pamoja na zashule wakati wote awapo shuleni.

(iii) Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo katika mazingira ya shule na anaposafiri wakati wa likizo.

(iv) Kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote iliyoanishwa katika ratiba ya shule.

(v) Kuhudhuria maandalio ya jioni(preparation) ya kila siku bila kukosa ili kujiandaa vyema namitihani na majarabio yote ikiwemo mithani ya Taifa.

(vi) Kutunza, kuheshimu na kuthamini mali za shule, mali za wenzake pamoja na mali zake mwenyewe kwa kuhakikisha kila kifaa mfano, madawati, meza, vifaa vya usafi n.k vimehifadhiwa mahali panapotakiwa na katika hali ya usafi.

(vii) Kutii na kuitika mara asikiapo mlio wa kengele inayomtaka afanye jambo fulani lililoelekezwa katika ratiba ya shule.

(viii) Kupata milo yote ya chakula bila kukosa kwa kisingizio chochote kama siyo ugonjwa ambao umethibitishwa na daktari.

(ix) Kuhudhuria masomo yote yafundishwayo darasani bila kukosa wala kuchelewa.

(x) Kulinda na kufanya usafi wa mazingira ya shule kulingana na taratibu na mpangilio uliowekwa na shule na awe tayari kukaguliwa na wahusika.

(xi) Kutotupa taka hovyo, kuokota taka zilizotupwa hovyo na kuhifadhi katika pipa lataka katika eneo husika.

(xii) Kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi wa baraza la wanafunzi bila ubishi wala manung’uniko na kufuata maelekezo yote yatolewayo na walimu pamoja naviongozi wa baraza la wanafunzi.

(xiii) Kuhudhuria ibada na sala kwa muda uliopangwa na katika eneo husika kwa dhehebu lake kulingana na ratiba na taratibu za shule.

(xiv) Kutunza na kuheshimu muda kwa kutembea haraka/kukimbia wakati wote anapoelekea eneo lolote ndani ya shule au nje ya shule.

(xv) Kutunza nishati ya umeme kwa kuzima taa baada ya kumaliza matumizi yake. Mf. Madarasani, na mabwenini.

(xvi) Kutunza maji kwa kufunga bomba baada ya kumaliza matumizi yake.

(xvii) Kufanya mazoezi ya viungo kulingana na ratiba ya shule pasipo kisingizio chochote isipokuwa ugonjwa uliothibitishwa na dakitari au muuguzi wa shule.

- **WAJIBU WA MZAZI**

Kila mzazi mwenye mwanafunzi katika shule ya Sekondari ya Omumwani ana wajibu ufuatao kwamwanaye na kwa shule:

(i) Kulipa ada na michango yote kwa ajili ya masomo ya mwanae kwa wakati nakwa kiwango kilichoanishwa katika barua ya kujiunga na shule na makala nyingine zinazotumwa kwa wazazi kila muhula.

(ii) Kushirikiana na walimu na walezi kufuatilia na kudhibiti mwenendo na tabia yamwanae kwa kutoa maonyo na makaripio kwa wakati muafaka kadri atakavyotakiwa au kuelekezwa na uongozi wa shule.

(iii) Kushirikiana na walimu kufuatilia taaluma ya mwanae kwa kumpa mahitaji muhimu na mazingira salama ya kumuwezesha kusoma kwa utulivu, kutoa karipio endapo maendeleo ya kitaaluma ya mtoto sio mazuri pamoja na kushirikikubuni na kutekeleza mbinu bora za kuongeza kiwango cha ufaulu kwa mwanae

(iv) Kuhakikisha mwanae anapata malezi bora wakati wote awapo nyumbani kwa kudhibiti tabia ya uvivu na uzururaji inayosababisha wanafunzi kujiunga katika makundi mabaya na hatimaye kuwasababisha kuiga tabia mbaya na kujiingiza katika mazingirahatarishi.

(v) Kupata ripoti ya maendeleo ya Taaluma ya mtoto wake kwa wakati muafaka.

Mzazi ambaye hatatimiza wajibu wake ipasavyo atasababisha matatizo na usumbufu kwake na mwanae kwani mwanafunzi atarudishwa nyumbani hadi hapo mzazi atakapoonesha ushirikiano wa dhati katka malezi ya mtoto wake.

**Hivyo mzazi timiza wajibu wako kwa wakati bila kusubiri kukumbushwa kwa faida yako, ya mwano na Taifa kwa ujumla.**

- **TARATIBU NA KANUNI ZA KILA SIKU.**

Taratibu na kanuni hizi zimewekwa ili zifuatwe na kila mwanafunzi bila kusita na kwa wakati wote awapo shuleni. Kukiukwa kwa taratibu na kanuni hizi kutamsababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali ikiwemokurudishwa nyumbani.

i) Mwanafunzi avae sare za shule wakati wote awapo shuleni na wakati wa kwenda nyumbani au kurudishuleni.

ii) Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa kandambili au viatu vya aina nyingine wakati akiwa katika sare rasmi ya shule tofauti na viatu alivyoagizwa.

iii) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa iliyoidhinishwa na mkuu wa Shule,makamu mkuu wa shule na mwl wa nidhamu.

iv) Ni marufuku kabisa mwanafunzi kuingia kwenye nyumba ya mtumishi yeyote bila kibali au ruhusarasmi.

v) Ikiwa mwanafunzi ana matatizo ya kinidhamu, kifamilia ua ugonjwa ni mzazi/mlezi pekee ambaye picha yake ipo katika maelezo ya mwanafunzi atakayewajibika kufika shuleni kumchukua, kusikilizwa, na kujadiliana na walimu kuhusu nidhamu au ugonjwa wa mwanaye. Mtu mwingine yeyote yulehatakabidhiwa wala kujadili matatizo ya mtoto asiye wake.

vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kulala katika kitanda na bweni alilopangiwa muda wote awapo shuleni.

vii) Mwanafunzi harusiwi kuhama bweni au kulala wawili ni kosa kubwa na akigundulika ataadhibiwavikali.

viii) Vyakula na milo yote iliwe katika bwalo la chakula na vifaa vya chakula vitunze vizuri . (Ni kosakubwa mwanafunzi kukutwa na chakula bwenini).

xi) Kila mwanafunzi anatakiwa kupata mlo wake katika meza yake aliyopangiwa na atawajibika kuisafishakila baada ya mlo kwa utartibu waliojiwekea.

x) Jikoni ni mahali pa kupikia chakula hivyo panatakiwa kuwa safi wakati wote. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni bila sababu ya msingi na atatakiwa kuingia eneo la chakula akiwa amevaa viatu vya kufungwa na kamba.

xi) Vifaa vyote vya umeme kama vile simu, redio, pasi, kamera n.k, haviruhusiwi kwa mwanafunzi anapokuwa shuleni.

xii) Vipodozi, manukato makali (perfumes) n.k haviruhusiwi kwa mwanafunzi awapo shuleni.

xiii) Mwanafunzi atakayelazimika kulala kwa ajili ya ugonjwa ni lazima apate uthibitisho wa daktari au nesi wa shule kupitia kwa matron.

xiv) Atakayeugua akiwa darasani na kuhitaji kupata matibabu katika zahanati ya shule anatakiwa kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa au wa zamu.

xv) Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa masomo mpaka kwa kibali maalumu kutokakwa mkuu wa shule aidha siku za **Jumamos na jumapili haturuhusu**

**wageni**.

xvi) Mwanafunzi anayetoka likizo anatakiwa kuripoti shuleni si zaidi ya saa 10:30 jioni tofauti na hapo maelezo ya kina yatatakiwa kutoka kwa mzazi ikiwemo na mwanafunzi kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

- **MAKOSA YATAKAYOMSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE MARAMOJA NI PAMOJA NA;**

(i) Wizi wa mali ya shule au ya mwanafunzi mwenzake.

(ii) Kuingia na SIMU au CHIP (line) ya simu shuleni au kukutwa akiongea na simu yamtumishi bila kupata kibali cha Mkuu wa shule/ Makamu Mkuu wa shule.
**(mzazi /mlezi usimpe mwanao simu kwa kisingizio chochote kile haitakubalika) kwa mawasiliano ya dharula tafadhali tumia namba za simu za matron zilizotajwa kwenye fomuhii kwa siku za Jumatano na Ijumaa**

(iii) Uasherati na uzinzi nje na ndani ya shule.

(iv) Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya.

(v) Kuingia mahali panapouzwa kileo/pombe

(vi) Kuvuta sigara, kutafuna mirungi na kuvuta ugoro.

(vii) Kutoa lugha ya matusi hadharani au kwa kificho kwa walimu na wanafunzi wenzake.

(viii) Kupigana hadharani au kutishia kumpiga mwanafunzi mwingine kwa sababu yoyote ile.

(ix) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, miundombinu ya shule au mali za wanafunzi wenzake.

(x) Kupata au kutoa ujauzito.

(xi) Utoro kuanzia siku moja na kuendelea, mwanafunzi kulala nje ya shule baada ya kupewa ruhusa yakutwa.

(xii) Kuingia katika nyumba ya watumishi pasipo ruhusa maalumu.

(xiii) Kuchochea au kushiriki katika mgomo wowote au mikutano isiyo rasmi.

(xiv) Kuingia shuleni na vyakula apewapo ruhusa au arudipo kutoka likizo.

(xv) Kugomea adhabu halali iliyotolewa na viongozi wa baraza la wanafunzi, kiongozi wadarasa, mwalimu au mtumishi yeyote mwenye mamlaka.

(xvi) Kutohudhuria masomo darasani kwa muda wa siku 90 mfululizo.

(xvii) Kutenda tendo lolote lisilo la kawaida shuleni au nje ya shule.

**Kila mzazi/mlezi asome kwa makini sheria na taratibu hizi akiwa na mwanaye na ahakikishe amemsaidia mwanaye kuzielewa kwa ajili ya kuzifuata kwa makini. Baada ya kuzielewa, mzazi na mwanafunziwasaini kukubaliana nazo pamoja na adhabu zinazoambatana nazo. Mzaziatoe nakala mbili (2) za sheria hizi, nakala moja ibaki na mzazi nakala halisi irudishwe shuleni na nakala moja ibaki na mwanafunzikwa ajili ya kujikumbusha kila siku.**

## AHADI YA MZAZI

Mimi ……………………………………………… Mzazi/Mlezi wa .................................. nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na sote kwa pamoja tumezielewa. Ninakubali kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizo.

## AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi ……………………………………….. Wa kidato cha ………………………………
Nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na mzazi wangu. Nimejadiliana naye na nimezielewa vizuri kabisa. Ninaahidi nitazifuata endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

Saini ya mzazi ……………………………………….. Tarehe …………………………
Saini ya mwanafunzi ………………………………… Tarehe …………………………

**Ni imani yangu kuwa utafuata taratibu hizi ili uweze kujifunza kwa bidii kwa mafanikio yaliyo bora.Nakutakia kila la heri na karibu sana Omumwani Sekondari.**

**NB**: PRINT PICHA YENYE RANGI (COLOURED) ILI KUONA RANGI HALISI YA SARE YA SHULE.





## ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI

### ADVANCED

- Conceptual Advanced Mathematics for secondary schoo F V+ VI Author
- Advanced Mathematics for advanced level (TIE). Form five and form six.

### PHYSICS

- Principles of Physics Class XI (CHAND)
- Principles of Physics Class XII (CHAND)
- Advanced physics form five (TIE)
- Advanced physics form six (TIE)

### CHEMISTRY

- Conceptual chemistry (CHAND)
- Physical chemistry, General chemistry, Organic chemistry & In organic chemistry(TIE)
- Inorganic chemistry part 1 & 2 (TIE)
-

### BIOLOGY

- Vema PS & Pandey B.P (2006) S.CHAND'S Biology for class XI. 2nd multiocoloure.d.S.Chand & company Ltd New Delhi.
- Biology functional approach 4th Edition, Biology form V & VI, TIE

### GEOGRAPHY

- **Zisti Kamili (2016) PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVE**
- TIE (2022) Practical Geography for Advanced secondary schools. Student's book. Form five and six.
- TIE (2022) Physical Geography for Advanced secondary schools. Student's book. Form five and six.
- Preparation forAdvanced Certificate of secondary Education Examination Geography Map Sheets & Photographs. Advanced students (**Compulsory**)

**HISTORY**

- How Europe underdevelop Africa (water Radney) ***Advanced level History two.***
- Bigirwamungu I and Deogratius.M (2015) ***Understand African History paper 1***
- ***Mwl. Kato (2009) A mastering advanced level history 1 & 2***
- ***Yasin, S (2010) Essential in advanced level History paper 2***

***OR***

- Shibitali, C.K.T (2010), ***Contemporary Historical events, Advanced levelHistory one***
- ***Kitabu cha history cha Bakari Madaya***

## ENGLISH LANGUAGE

### PLAYS (English)

- The government inspector Author Nikolai V. Gogol
- An Enemy of the people Author Henrik Ibsen
- A Teste of Heaven Author Farouk Topan

### NOVELS (English)

- Animal farm Author George Orwell
- Chasing the Leopard finding the lion Author Julie wakeman-Linn
- The Opportunist Elite Author Nyambari C. Nyangwine
- The Horizon Unveiled Author Fellowes Mwaisela

### POETRY (English)

- Summons: Poem from Tanzania Author Richard S. Mabala et al.
- Poets of Africa: Lament of the Silent & other Poems.

## LITERATURE IN ENGLISH

### Novel (literature in English)

- Arrow of God Author Chinua Achebe
- A Man of the people Author Chinua Achebe
- A Grain of Wheat Author Ngungi Wathiong'o
- Petals of Blood Author Ngungi Wathiong'o
- No Longer at Ease Author Chinua Achebe
- Joy Comes in the Morning Author Hopolang Phororo
- The Lion of Yola Author Severine Ndunguru

### Novel (literature in English)

- Betrayal in the city Author Francis Imbuga
- I will mary when I want Author Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii
- Julius Caesar Author William Shakespeare
- Man of kafira Author Francis Imbunga

### POETRY Novel (literature in English)

- Poets of Africa 7; Boundless Voices Poem From Kenya Author Arthur I Luvai
- The Bleeding Heart and Other Poems Author Shilia Kaaya

## KISWAHILI

### Riwaya (Kiswahili)

- Dunia Uwanja wa Fujo — Mwandishi Euphrase Kezilahabi
- Ua la Faraja — Mwandishi W.E Mkufya
- Mirathi ya Hatari — Mwandishi C.G Mung'ong'o
- Wasifu wa Siti Binti Saad — Mwandishi Shaaban Robert

### Tamthiliya (kiswahili)

- Mukwava wa Uhehe — Mwandishi M.M. Mulokozi
- Shujaa Mirambo — Mwandishi Emmanuel Mbogo
- Usaliti Mjini — Mwandishi Francis Imbuga

### Ushairi (Kiswahili)

- Fumbo Linaloelea — Mwandishi Nyambari C.M Nyangwine
- Malenga wa Ziwa kuu — Mwandishi Wallah Bin Wallah
- Andamo, Msafiri Safarini — Mwandishi Mohammed Khelef Ghassani
- Wosia wa baba — Mwandishi Ahmed Mohamed Amanzy

## FASIHI YA KISWAHILI

### RIWAYA (Fasihi ya Kiswahili)

- Vuta N'kuvute — Mwandishi Shafi Adam shafi
- Asali Chungu — Mwandishi Said Ahmed Mohamed
- Mwana wa Yungi Hulewa — Mwandishi Mohamed Said Abdulla
- Vipuli vya Figo — Mwandishi Emmanuel Mbogo

### TAMTHILIYA (Fasihi ya Kiswahili)

- Kaptula la Marx — Mwandishi Euphrase Kezilahabi
- Nyerere na safari ya Kanaani — Mwandishi Emmanuel Mbogo
- Morani — Mwandishi Emmanuel Mbogo

### USHAIRI (Fasihi ya Kiswahili)

- Dhifa — Mwandishi Euphrase Kezilahabi
- Utenzi Majumui wa karne ya 21 — Mwandishi Idd M. Mwimbe
- Malenga wa Bara — Mwandishi M.M Mulokozi na K.K Kahigi
- Fungate ya Uhuru — Mwandishi Mohamed Seif Khatibu

**ECONOMICS**

- Advanced Economy Book 1 & 2
- Advanced economy book form six (TIE)